***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA***

**OFISI YA RAIS,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MKOA WA NJOMBE

**MTIHANI KABLA YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA SITA**

**121/2** **KISWAHILI 2**

**(Kwa Watahiniwa wa Shule na Kujitegemea)**

**MUDA: SAA 03: 00** **IJUMAA, 15 Machi 2024 Mchana**

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B**
2. Jibu maswali **yote** kutoaka sehemu **A** na **Maswali (3)** kutoka sehemu **B**
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na kila swali.
4. Kumbuka kuandika namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa karatasi yako ya kujibia.

**SEHEMU A: (Alama 40)**

**FASIHI KWA UJUMLA NA USANIFU WA MANDISHI.**

Jibu Maswali yote katika sehemu hii

1. Uhai wa fasihi simulizi hujipambanua wakati wa uwasilishaji. Jadili kauli hiyo kwa hoja tano.

2. Kwa kuegemea mawazo ya wataalamu mbali mbali jadili dhana ya fasihi kwa hoja nne (4) na hitimisha kwa msimamo wako.

3. Fafanua athari chanya tano za udhamini wa kazi za fasihi kwa msanii.

4. Soma kifungu cha Habari kifuatacho kisha bainisha mbinu za kifani zilizo tumika.

    Matokeo ya mtihani ule ulimfanya arukwe na akili kwani yalikuwa ni kinyume kabisa na matarajio, matumaini na malengo ya Maisha yake.Alivuna alicho kipanda. Baada ya kutaabika kupanda na kulea mche ule kwa dhiki nyingi na ya muda mrefu, hatimaye amechuma shahada isiyo na tija kwake, kwa wazazi wake wala jamii yake. Nakila mchuma janga hula na wakwao.Aliona dunia na wote walio ikalia wanamdharau mithili ya dume zima lililojinyea hadharani.Hakuwa na chakujivunia tena akawa piritoni, kilicho mtia uchungu nikuona kwamba marafiki zake wa karibu wote walimtupa mkono;si Nyangaswa, Vanesa, Mama Doto wala Binti Cheupe, wote walianza kumuona kama kinyesi.Alipatwa na kijiba cha roho. Hasira, huzuni, fadhaa, aibu na hofu viliusakama moyo wake.Akaamua kujiweka mwenyewe mbele ya mahakama ya rohoni mwake ; akajiona kama aliyeketishwa mbele ya kiti cha hukumu cha mwenyezi Mungu, akajifanya hakimu tena mfawidhi akajisomea mashitaka.

    Kesi namba 00/01/02, Faili namba 01 ya mwaka huu. Mshitakiwa Masumbuko Sina unashitakiwa na serikali ya jamhuri,wazazi, ndugu, walimu na jamii yote kuwa kwa maakusudi kabisa, huku ukielewa fika kuwa gharama nyingi zimetumika kwa kukuzaa, kukulea na kukusomesha hadi ukafikia kuhitimu kidato cha ………. Ukafanya uzembe wa kutotumia akili zako vizuri kwa kupenda anasa kama ………. hata ukasababisha kupata daraja sifuri. Kutokana na matokeo hayo umelitia taifa hasara ya mamilioni ya fedha za ndani na za kigeni, umesababisha taifa ndugu na jamaa zako kukosa huduma kutoka kwako kama mtaalamu mtarajiwa;

    Hivyo mahakama hii imekubaini na kukutia hatiani kwa makosa yafuatayo,kwa mujibu wa sheria ya nchi namba 002/01 ya mwaka huu.Uzembe wa kuruhusu mwili wako hupenda usingizi badala ya kusoma, kuwadharau walimu wako, usaliti na uasi kwa imani yako ya dini ambayo inakataza uvivu kwa waumini wake wote nawe ukiwa mmoja wao, kulinyang'anya taifa makusudi pato lake na kuwaletea wazazi na ndugu simanzi na usumbufu wa makusudi ambao ungeweza kuepukika .

    Hivyo kutokana na makosa hayo mahakama haina budi kutoa adhabu kali kwako ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia na mwenendo kama wa kwako waache mara moja.Loo! kumbe alikuwa katika mawazo alishituliwa na rafiki yake aliyekuwa akigonga mlango wa chumba chake ili kumjulia hali, kwa sauti iliyosikika jamaa! Jamaa! nje ya mlango wake.

**SEHEMU B: (Alama 60)**

**FASIHI ANDISHI**

Jibu Maswali **matatu (03)** katika sehemu hii, swali la **tano (05)** ni la lazima

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

Kimbunga - Haji gora
Mapenzi bora - Shabani Rob
Fungate ya Uhuru - Mohamed S. Khatib

**RIWAYA**

Usiku utakapokwisha - Mbunda Msokile
Kufikirika - Shabani Robert
Mfadhili - Hussein Tuwa
Vuta N'kuvute -Shafi Adam Shafi

**TAMTHILIA**

Kwenye ukingo wa Thimu - Ebrahim Hussein
Morani - Emanuel Mbogo
Kivuli Kinaishi - Said Mohammed
Nguzo Mama - Penina Muhando

5. ''Mwandishi ni kichocheo cha maendeleo katika jamii '' eleza mchango wa washairi katika kuleta maendeleo, kwa kwa kutumia hoja nne kwa kila kitabu, kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

6. Lugha ni kibebeo cha kazi ya fasihi, pasipo kuwa na matumizi mazuri ya lugha kazi ya fasihi haijajengeka na hakuna fasihi. Kwa kuzingatia kauli hiyo eleza matumizi ya tamathali za semi za mlinganisho kutoka katika diwani mbili ulizo soma, hoja tatu kutoka katika kila diwani.

7. ''Elimu ni ufunguo wa maisha'' Fafanua kauli hiyo kwa kurejelea mambo ambayo umeelimishwa kutoka katika riwaya mbili ulizo soma, kwa hoja nne kutoka katika vitabu ulivyo soma.

8. ''Waandishi huwajenga wahusika katika hali zinazoweza kuibua hisia za wasomaji kuwachukia wahusika wao kutokana na matendo wanayotenda" thibitisha kauli hiyo kutoka katika tamthiliya mbili ulizosoma kwa hoja nne kutoka katika kila kitabu.